

# MANENO MATAMU


Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal

**MUHAMMAD ILYAS**

**Attar Qadiri Razavi**

مِیٹھے بَول

Meethay Bol

# MANENO MATAMU

HII HOTUBA ILITOLEWA NA Shaykh-e-Tareeqat, Ameer-e-Ahl-e-Sunnat, mwanzilishi wa Dawat-e-Islami 'Allamah Maulana Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qaadiri Razavi دَامَتۡ بَرَکَاتُہُمُ الۡعَالِیَہ kwa kiurdu. **Translation Department** (Idara ya tafsiri) imetafsiri kwenda kiswahili.Ukipata kosa lolote kwenye tafsiri au utungaji, tafadhali wataarifu idara ya tafsiri juu ya zifuatazo anuani za posta au barua pepe kwa nia ya kupata thawab [Sawab].

**Translation Department (Dawat-e-Islami)**

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran, Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

**UAN:** ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 7213

**Barua pepe:** 🖃 translation@dawateislami.net

**Maneno matamu**

**Tafsiri ya kiswahili ya** 'Meethay Bol'

◆

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA

Hakimiliki © 2023 Maktaba-tul-Madinah

Hakuna sehemu ya chapisho hili inaweza kutolewa tena, au kupitishwa kwa njia yeyote au kwa maana yeyote, umeme, mitambo, nakala, kurekodi na vinginevyo bila ya ruhusa ya awali ya maandishi ya Maktaba-tul-Madinah.

**Uchapishaji wa kwanza:** Ramaḍān-ul-Mubārak, 1448 AH– (March, 2023)

**Kimetafsiriwa na:** Translation Department (Dawat-e-Islami)

**Mchapishaji:** Maktaba-tul-Madinah

**Idadi:** 3000

## UFADHILI

Jiskie huru kuwasiliana nasi kama unapenda kudhamini uchapishaji wa vitabu vya dini au kijitabu kwa ajili ya sadaka za wanafamilia waliotangulia mbele za haki (marehemu)

**Maktaba-tul-Madinah**

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah Mahallah Saudagran,
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

✍**Barua pepe:** maktabaglobal@dawateislami.net –
maktaba@dawateislami.net

✆ **Namba za simu:** +92-21-34921389-93

💻 **Tovuti:** www.dawateislami.net

# *JEDWALI LA YALIYOMO*

**Maneno matamu*** ........ 1
Moja ya sababu za adhabu katika kaburi ........ 1
Maneno matamu ........ 4
Kipande cha nyama ........ 5
Malipo ya ibada ya mwaka mmoja kwa kila neno ........ 5
Baraka za maneno matamu ya waja wa Mtume ﷺ ........ 6
Habari njema ya msamaha ........ 9
Matendo ya kupata nafasi mbinguni ........ 10
Kufyonzwa! ........ 10
Kupanda miti ........ 11
Dhambi za miaka 80 zimesamehewa ........ 12
Hairuhusiwi kusema 'Bismillah ki-jiye' ........ 13
Wakati gani ni Kufr kusema 'بِسْمِ اللّٰه'? ........ 14
Wakati gani ni dhambi kufanya Zikrullah? ........ 14
Kuita Haleem [حَلِيْم] badala ya Khichra ........ 15
Nyakati za malipo laki moja ........ 16
Ubora wa kutimiza hitaji na kuuliza juu ya afya ya mtu ........ 16
Malipo makubwa ya kuuliza juu ya afya ya mtu ........ 17
Jozi ya mavazi ya Mbinguni ........ 18
Ulimi una faida na pia unadhuru ........ 18
Kila asubuhi sehemu za mwili huomba ulimi ........ 18



www.dawateislami.net

Matatizo yanayosababishwa na matumizi mabaya ya ulimi .............. 19
Furaha ya milele na karaha .................................................................. 20
Matokeo ya ugumu wa moyo ............................................................... 21
Kusagwa ulimi! ....................................................................................... 22
Mtu anapaswa kufanya nini juu ya kusema kitu bila ya lazima? ....... 23
Mifano 14 ya sentensi zisizo za lazima ................................................ 24
Mifano 13 ya maswali yasiyo ya lazima yaliyoulizwa kutoka kwa Hujjaj. 26
Mifano 4 ya sentensi mbaya au za dhambi .......................................... 27
Mifano 19 ya maswali yasiyo ya lazima yaliyoulizwa siku ya Eid-ul-Adha ........................................................................................................ 28
Mifano 5 ya mazungumzo yasiyo ya lazima yaliyofanywa wakati wa kuzungumza kwenye simu .................................................................. 29
Mifano14 ya maswali yanayomlazimisha mtu kusema uwongo .......... 30
Maneno hatari zaidi yasiyo ya lazima ................................................. 31
Ufafanuzi wa "taarifa isiyo ya lazima" ................................................. 33
Watu wa ajabu wa kuongea .................................................................. 35
Kuchambua mazungumzo ...................................................................... 36
Lulu za Madani 12 kuhusu kuingia na kutoka nyumbani .................. 38



www.dawateislami.net

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَ الصَّلٰوةُ وَ السَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

## Du'a kwa ajili ya kusoma kitabu

Soma Du'a ifuatayo (Dua) kabla hujasoma kitabu cha kidini au mafunzo ya kiislamu, utakumbuka chochote unachosoma, اِنْ شَآءَ اللّٰه عَزَّوَجَلَّ:

اَللّٰهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْاِكْرَام

Tafsiri Ewe mwenyezimungu عَزَّوَجَلَّ**! Tufungulie mlango wa maarifa na hekima, na utuhurumie! Ewe Mwenye heshima na utukufu zaidi!**

*(Al-Mustatraf, vol. 1, p. 40)*

**Kumbuka:**

soma Salat-'Alan-Nabi ﷺ mara moja kabla na baada ya Du'a



www.dawateislami.net

**Mwanga mkuu wa kiroho na kitaaluma** wa karne ya 21, 'Allamah Maulana **Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qaadiri Razavi** دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَه ameanzisha **Dawat-e-Islami** (harakati za kimataifa na zisizo za kisiasa kwa ajili ya mahubiri ya Quran na Sunnah) ambayo inaeneza mafunzo ya kiislamu katika Zaidi ya nyanja 100 za maisha.Ukitaka kujua kuhusu mwanzilishi wa Dawat-e-Islami, vitabu vyake, vijitabu, na idara mbalimbali za Dawat-e-Islami, basi tembelea hii tovuti: www.dawateislami.net.

Zaidi ya hayo, Dawat-e-Islami pia inaeneza ujumbe wa kiislamu duniani kote kwa Idhaa ya **Madani**, (Madani Chanel) Kwa asilimia 100 (100%) kabisa idhaa ya kiislamu. Bila kujali popote ulipo duniani, ikiwa una nia ya kutazama Madani Chaneli, kisha fuata masafa uliyopewa. Ukitaka kuwasiliana nasi, basi tutumie barua pepe: overseas@dawateislami.net

## Madani Chaneli (idhaa ya madani)- Vigezo vya Chanjo ya Kimataifa

### Uambukizaji: Kidijitali

| Satelaiti | Aina ya boriti | Nafasi | Kiungo cha chini | Hz. | Polarity | Kiwango cha mfumo | FEC |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Asiasat (A7-C3V) | Kimataifa | 105.5 E | C-Bendi | 3739 | Wima | 2815 | 3/4 |
| Intelsat 20 | Mikoa ya Africa | 68.5 E | KU-Bendi | 12562 | Mlalo | 26657 | 2/3 |
| Eutelsat 7 | Mashariki ya kati | 7 Magharibi A | KU-Bendi | 10815 | Mlalo | 27500 | 5/6 |
| Astra 2F | Ulaya | 28.5 E | Jukwaa la anga | 12640 | Wima | 22000 | 5/6 |
| Galaxy 19 | Marekani | 97 Magharibi | KU-Bendi | 121835 | Mlalo | 22000 | 3/4 |

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِیْنَ وَ الصَّلٰوةُ وَ السَّلَامُ عَلٰی سَیِّدِ الْمُرْسَلِیْنَ
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّیْطٰنِ الرَّجِیْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ ؕ

# Maneno matamu*

Shetani pengine atakuzuia kusoma kijitabu hiki kabisa lakini unapaswa kuzuia majaribio yake.

## Moja kati ya sababu za adhabu za kaburi

Imenukuliwa katika '*Al-Qaul-ul-Badi*' kwamba Sayyiduna Abu Bakr Shibli Baghdadi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Niliota kuhusu marehemu jirani yangu na nikamuuliza, 'مَا فَعَلَ اللّٰهُ بِكَ' i.e. Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ alikutendeaje?' Alijibu: Nilikumbana na magumu makubwa. Hata sikuweza kujibu maswali ya Munkar wa Nakeer[1]. Nilijiwazia moyoni kuwa labda sijafa katika hali ya Iman! Maana nilisikia sauti, 'Unaadhibiwa kwa kutumia ulimi wako duniani pasipo ulazima'

Kisha malaika wa adhabu wakanisogelea lakini wakati huo

---

* Ameer–e-Ahl-e-Sunnat دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَه alitoa hotuba hii katika Ijtima' ya kila wiki yenye msukumo wa Sunnah (mkusanyiko) wa Dawat-e-Islami, harakati za kimataifa zisizo za kisiasa za Qur'ani Tukufu na Sunnah, katika Aalami Madani Markaz Faizan-e-Madinah in Rabi'-un-Noor, 1430 AH, 2009. Inachapishwa na marekebisho madogo. [Majlis Maktaba-tul-Madinah

[1] Malaika wawili wanaouliza maswali kaburini.

huo, mtu mzuri sana aliyenukia manukato mazuri sana alionekana kati yangu na mateso.Alinifanya nikumbuke majibu ya maswali ya Munkar wa Nakeer nami nikamjibu ipasavyo. اَلْحَمْدُلِلّٰہ عَزَّوَجَلَّ! Mateso yaliondolewa kwangu. Nilimuuliza kwa unyenyekevu mtu yule mheshimiwa, 'Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ akuhurumie. Wewe ni nani?' Alijibu,'Nimeumbwa kwa fadhila za tendo lako la kuzituma Salat-'Alan-Nabi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kwa wingi na nimepewa kazi ya kukusaidia katika kila shida.' *(Al-Qaul-ul-Badi', p. 260)*

*Aap ka naam-e-naami ay* صَلِّ عَلي
*Her jagah her museebat mayn kaam aa gaya*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب     صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

سُبْحٰنَ اللّٰہ عَزَّوَجَلَّ! Kama malaika anaweza kutusaidia kaburini kwa nguvu ya kutuma Salat-'Alan-Nabi kwa wingi, basi bwana wa malaika wote hakika anaweza kutusaidia na kutubariki!

Mtu aliomba kwa haki:

*Mayn gaur andhayri mayn ghabra`oon ga tanha*
*Imdaad mayri kernay aa jana mayray Aqa*

*Roshan mayri turbat ko Lillah Shaha kerna*
*Jab waqt-e-naz'a aaye deedar 'ata kerna*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب     صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

Mtakatifu aliyebarikiwa رَحْمَةُاللّٰہِ عَلَیْہ of Khurasan aliamriwa katika ndoto yake kualika taifa la Tatar kuelekea uislamu.

Wakati huo Tagudar Khan, mtoto wa Halaku Khan alikuwa mtawala. Mtakatifu huyo aliyebarikiwa رَحْمَةُاللّٰہِ عَلَیْہ alianza mkutano na Tagudar Khan. Kwa kumuona muislamu huyu mwenye ndevu Muballigh (mhubiri) ambaye alikua mfuasi wa kweli wa Sunnah, Tagudar Khan alihisi kufanya mzaha na kusema, 'Niambie kama nywele za ndevu zako ni bora au mkia wa mbwa wangu?' Hakika sentensi hii ingemkasirisha mtu mwingine yeyote lakini tangu mtakatifu aliyebarikiwa رَحْمَةُ اللّٰہِ عَلَیْہ alikua Muballigh mwenye busara, alijibu kwa upole sana, 'Mimi pia ni mbwa wa muumba wangu, (Allah) عَزَّوَجَلَّ. Mimi ni bora ikiwa nitafaulu kumpendeza kwa uaminifu wangu na kujitolea; vinginevyo mkia wa mbwa wako ni bora kuliko mimi kama mbwa wako atabaki kuwa mtiifu na mwaminifu kwako.'

Alikua anafanya mazoezi Muballigh ambao wangejiepusha na tabia mbaya kama kusengenya, kusimulia hadithi, kutafuta makosa kwa wengine, kutumia lugha chafu, kuzungumza kupita kiasi, na kila mara angeuweka ulimi wake katika Dhikrullah عَزَّوَجَلَّ. Kwa hiyo, maneno yake matamu yalikua na athari kubwa kwenye moyo wa Tagudar Khan. Aliposikia lulu tamu za madani kutoka kwa mazoezi ya Muballigh kwa kujibu swali lake la kipuuzi, aliona aibu na kusema kwa upole, 'Wewe ni mgeni wangu, kwa hivyo tafadhali kaa nami.'

Kwa hiyo, رَحْمَةُاللّٰہِ عَلَیْہ akakaa nae.Tagudar Khan alikua akimtembelea kila usiku na mtakatifu aliyebarikiwa رَحْمَةُاللّٰہِ عَلَیْہ angemwita kuelekea



www.dawateislami.net

kwenye haki na kwa adabu sana. Juhudi zake za kuendelea zilileta mapinduzi ya madani katika moyo wa Tagudar Khan. Tagudar Khan, yule yule aliyekuwa hapo awali na nia mbaya ya kuuondoa kabisa uislamu duniani, sasa ameanza kuupenda uislamu. Tagudar Khan aliukubali uislamu pamoja na taifa lake lote la Tatar mikononi mwa Muballigh huyu anayefanya mazoezi. Aliitwa 'Ahmad' baada ya kuukubali uislamu. Niukweli wa kihistoria kwamba jimbo katili la Tatar liligeuka kuwa milki ya kiislamu ya Asia ya kati kwa fadhila ya maneno matamu ya Muballigh.

Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ amhurumie na atusamehe kwa ajili yake!

اٰمِيْن بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَآله وَسَلَّم

## Maneno matamu

Ndugu wapenzi wa kiislamu! Uligundua kuwa Muballigh lazima awe na sifa kama hizo! Haya matokeo ya madani yasingeshuhudiwa kamwe kama angekua na hasira kwa swali la kipuuzi la Tagudar Khan.

Kwa hiyo, haijalishi hasira kiasi gani mtu hutufanya tujiskie, tunapaswa kuwa na udhibiti kamili wa ulimi wetu kwa sababu wakati fulani, hata hali ya kushinda inageuka kuwa hasara ikiwa ulimi hutoka katika udhibiti.Ilikua ni adabu ya maneno matamu ambayo ilimpa Tagudar Khan, utu na heshima,

ambaye hapo awali alikua mtu katili mbaya Zaidi kuliko wanyama.

*Hay falah-o-kamrani narmi-o-aasani mayn*
*Her bana kaam bigar jata hay nadani mayn*

## Kipande cha nyama

Ndugu wapenzi wa kiislamu! Ingawa ulimi unaonekana kuwa kipande kidogo tu cha nyama, kwa hakika ni Baraka kubwa kwa mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ.Labda, ni mtu asiye na sauti pekee ndiye anayeweza kuelewa thamani ya Baraka hii. Kutumia ulimi ipasavyo inaweza kumwongoza mtu mbinguni ilhali matumizi yake mabaya yanaweza kumpeleka motoni. Hata kama Kafir (asiye muislamu) mbaya atasema 'لَا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰه صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّم' huku ulimi wake ukiwa na Imani ya uislamu moyoni mwake, anakua ametakasika na uchafu wote wa Kufr na Shirk (ushirikina). Kalimah Tayyibah ambayo anasema kwa ulimi wake huosha dhambi zake zote za awali. Kwa wema wa kusema Kalimah Tayyibah kwa ulimi wake, anakua ametakaswa kabisa na dhambi, kana kwamba amezaliwa tu. Kusema Kalimah Tayyibah kwa ulimi wake wakati akiwa na Imani sawa ya moyo huleta mapinduzi haya makubwa ya Madani katika maisha yake.

## Malipo ya ibada ya mwaka mmoja kwa kila neno

Ikiwa tu watu wangejifunza kutumia ulimi wao ipasavyo.Mtu anaweza kumiliki nyumba peponi ikiwa atazungumza kwa

mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na Mtume wake kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Tutalipwa sana tukitumia ulimi wetu kwa kusoma Quran takatifu, kufanya Zikrullah[1], kwa wingi kutuma Salat na Salamu juu ya mtume mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, na kuita watu kuelekea kwenye haki, اِنْ شَآءَاللّٰه.

Imetajwa katika "*Mukashafa-tul-Quloob*"kwamba Sayyiduna Musa Kaleemullah عَلَيْهِ السَّلَام aliuliza kwa unyenyekevu mkuu kwenye mahakama ya Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ, 'Ewe Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ! Itakuaje malipo kwa mtu, anayemwita ndugu yake, anamuamuru kufanya matendo mema na kumzuia kutokana na matendo maovu?' akajibiwa, 'Ninaandika malipo ya ibada ya mwaka mmoja kwa kila neno lake na sitampa adhabu ya motoni.' *(Mukashafa-tul-Quloob, p. 48)*

## Baraka za maneno matamu ya waja wa Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّم

Ndugu wapenzi wa kiislamu! Si lazima mtu apate malipo kwa kutengeneza juhudi binafsi kwa kumwambia mtu kuhusu tendo la wema na kumfanya achukie dhambi, ikiwa tu atakubali na kutenda ipasavyo.Badala yake, اِنْ شَآءَاللّٰه kuna malipo makubwa hata asipokubali (wito kuelekea haki). Zaidi ya hayo, اِنْ شَآءَاللّٰه utapata faida kubwa katika dunia hii na akhera kama mtu akitubia dhambi zake na kuanza kufanya Sunnah kama matokeo ya juhudi zako binafsi.

---

[1] Kumkumbuka Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ.

Hapa ni mfano wa Madani wa juhudi za mtu binafsi katika suala hili.Ninataja dondoo (simulizi) iliyoandikwa ya ndugu mdogo wa kiislamu kutoka Kasur [Punjab, Pakistan] kwa maneno yangu mwenyewe: nilikua mwanafunzi wa darasa la kumi, kutumia maisha ya dhambi huku nikifurahia ushirika wa watu wabaya. Ningekasirika kirahisi sana na kuwadharau wengine vibaya sana. Ningewasema kwa ubaya si kwa baba yangu pekee, lakini kwa mababu zangu vilevile

Siku moja, Msafara wa madani (Madani Qafilah ya Dawat-e-Islami) – harakati ya kimataifa isiyo ya kisiasa ya Quran na Sunnah – ulifika kwenye msikiti katika eneo letu. Kwa Baraka za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ, Niliwatembelea waja hao wa mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Wakisafiri na Madani Qafilah. Huku akifanya juhudi binafsi, mmoja wao alinialika kujiunga kipindi cha Dars[1]. Nilichukua maneno yake matamu moyoni na kujiunga na kipindi.Baada ya Dars, huyo ndugu muislamu alinikaribisha kwa moyo mkunjufu kuhudhuria siku3 za mkusanyiko wa mafunzo ya Sunna (Sunnah-Ijtimaa) ambayo yangelifanyika hivi karibuni Sahra-e-Madinah katika Madina-tul-Awliya, Multan [Pakistan].Dars zake tayari zilinivutia, kwa hiyo sikuweza kukataa mualiko wake.

Nilipofikia eneo la Ijtima'Multan (panaitwa Sahra-e-Madinah), nilivutiwa na baraka na utulivu wa Ijtima'.Bayan ya mwisho (hotuba) ilikua juu ya uharibifu wa muziki [yenye jina *Gaanay*

[1] Hotuba ya Kiislamu

*Baajay ki Holnakiyan*] na iligusa moyo wangu.Nilitokwa na machozi na kabla sijatoka kwenye Ijtima', اَلْحَمْدُ لِلّٰه Nilitubia dhambi zangu zote na kujiunga na mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islami.

Kwa familia yangu, ni faraja kuona nikichukua mabadiliko ya haki ya Madani ya Dawat-e-Islami katika maisha yangu, ilivutiwa na mapinduzi ya Madani yaliyokumbatiwa na mtu asiye na adabu kama mimi na kwa baraka za mazingira ya Madani, kaka yangu mkubwa nae aliupamba uso wake na ndevu na kichwa chake na 'Imamah [kilemba cha Kiislamu]. Nina dada mmoja tu اَلْحَمْدُلِلّٰه na yeye pia alianza kuvaa burqa Madani'.

اَلْحَمْدُ لِلّٰه! Kila mtu wa nyumbani kwangu ameingizwa kwenye Qadiriyyah, Razawiyyah Tareeqah [i.e. utaratibu wa kiroho], hivyo kuwa Murideen [i.e. wanafunzi] wa Ghaus-e-A'zam رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه. Nina deni kwa ndugu huyo wa Kiislamu ambaye maneno yake matamu yalisababisha matokeo makubwa kama haya.Kwa neema za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ, nilimaliza kuihifadhi Quran takatifu.Zaidi ya hayo, nilijiandikisha kwa kozi ya Dars-e-Nizami ili kuwa mwanazuoni wa Kiislamu.

Wakati wa kuandika dondoo hii, niko katika mwaka wa tatu wa masomo yangu ya Dars-e-Nizami. اَلْحَمْدُلِلّٰه, Mimi pia ninasimamia Madani Qafilah katika eneo langu na kuanzia mwezi wa Sha'ban-ul-Mu'azzam 1427 Hijria, ninakusudia kusafiri kwa muda wa miezi kumi na mbili mfululizo pamoja na Madani Qafilahs.

*Dil pay ger zang ho, ghar ka ghar tang ho*
*Hoga sab ka bhala, Qafilay mayn chalo*

*Aysa fayzan ho, Hifz-e-Quran ho*
*Ker kay himmat zara, Qafilay mayn chalo*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Habari njema ya msamaha

Tumia ulimi wako kwa kusoma Qur'ani tukufu na upate malipo makubwa.

Hadeethul-Qudsi ifuatayo imetajwa katika kitabu 'Ruh-ul-Bayan':

Yeyote anayesoma Surah Al-Fatihah mara moja katika muendelezo wa بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ (i.e. 'بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ', mpaka mwisho wa Sura), basi uwe shahidi kwamba mimi nimemsamehe, nimekubali matendo yake mema yote, nimemsamehe madhambi yake, hakika sitauchoma ulimi wake na nitamuokoa kutokana na adhabu ya kaburi, moto wa Jahannam na adhabu ya Siku ya Kiyama na khofu kubwa.

*(Ruh-ul-Bayan, juzuu ya 1, uk. 9)*

Njia iliyo wazi zaidi ya kuzisoma Aya zote mbili zilizotajwa hapo juu kwa muendelezo imeonyeshwa katika yafuatayo:

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ

(Soma sura kamili).



www.dawateislami.net

## Matendo ya kupata nafasi mbinguni

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Omba 'اَسْتَغْفِرُ اللّٰہَ الْعَظِیْم' kwa ulimi wako na upate Hoor Mbinguni. Katika 'Raud-ur-Riyaheen', imetajwa: Waliyullah (Mtukufu aliyebarikiwa رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه )alikuwa amemuabudu Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ kwa muda wa miaka 40. Mara moja alifanya Du'a [i.e. dua], 'Ewe Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ! Tafadhali nifanye niwe na taswira katika ulimwengu huu wa kitu chochote kutoka katika yale yote nitakayotunukiwa Mbinguni kwa baraka Zako."Akiwa bado anafanya Du'a, ghafla Mihrab[1] iligawanyika na Hoor (Mwanamke mzuri kupidukia akatokea kutoka humo.Alisema, 'Mtalipwa Mbinguni Hoors 100 kama mimi, kila mmoja wao atakuwa na watumishi 100 wa kike, na kila mjakazi atakuwa na vijakazi 100 na kila kijakazi atakuwa na wasimamizi 100 wa kike.'

Waliyullah (Mtakatifu huyo) aliyebarikiwa رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه alifurahi sana baada ya kusikia na kuuliza, 'Je, kuna yeyote atapata hata zaidi kuliko mimi huko Mbinguni?'Akajibiwa, 'Kila mtu anayesoma اَسْتَغْفِرُ اللّٰہَ الْعَظِیْم' asubuhi na jioni, atabarikiwa na malipo haya mbinguni.' *(Raud-ur-Riyaheen, p. 55)*

## Kufyonzwa!

Daima husisha ulimi huu katika Dhikr za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ kupata malipo makubwa.Mtume wetu Mpendwa

[1] Ile sehemu ya Msikiti ambapo Imam anasimama katika Swalah ya jamaa.

صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alisema: Fanya Dhikr za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ kiasi kwamba watu wanaanza kukuita (wewe) kichaa.

*(Al-Mustadrak lil-Haakim, vol. 2, p. 173, Hadith 1882)*

Imeelezwa katika Hadithi nyingine: Fanya Zikr za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ kiasi kwamba wanafiki waanze kukuita unajionyesha (show-off). *(Al-Mu'jam-ul-Kabeer, vol. 12, p. 131, Hadith 12786)*

## Kupanda miti

Mtume wetu mpendwa صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alimwambia Sayyiduna Abu Hurayrah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ kuhusu matumizi makubwa ya ulimi yenye manufaa.Soma na ufurahi:

*Imepokelewa katika riwaya ya Sunan Ibn Majah* kwamba (mara moja) Mtume wetu mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikua anaenda mahali fulani.Alimuona Sayyiduna Abu Hurayrah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ kupanda mmea.Mtume wetu mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم Akauliza, "Unafanya nini?" Akajibu kwa unyenyekevu, "Mimi napanda mti! Mtume wetu wa rehma صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasema: Acha nikuambie njia ya kupanda mti bora, Mti mmoja hupandwa Mbinguni kama malipo ya kila neno kwa kukariri. سُبْحٰنَ اللهِ وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ وَلَا اِلٰهَ اِلَّا اللهُ وَ اللهُ اَكْبَر.'

*(Sunan Ibn Majah, p. 252, vol. 4, Hadith 3807)*

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Katika Hadithi zilizotajwa hapo juu,



www.dawateislami.net

maneno manne yameelezwa: (1) سُبْحٰنَ اللّٰهِ, (2) اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ, (3) لَا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ, (4) اَللّٰهُ اَكْبَر. Miti minne itapandwa Mbinguni ikiwa utasoma maneno yote manne na miti michache itapandwa ikiwa utasoma kidogo.Kwa mfano, mti mmoja utapandwa ikiwa 'سُبْحٰنَ اللّٰهِ' itasomwa. Endelea kukariri maneno haya kwa ulimi wako na uendelee kupanda miti zaidi na zaidi Mbinguni.

عُمر را ضائِع مَکُن در گفتگو ذِکرِ اُوکُن ذِکرِ اُوکُن ذِکرِ اُو

(i.e. usipoteze maisha yako ya thamani kwa kufanya mazungumzo yasiyo ya lazima.Fanya Zikr za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ, fanya Zikr za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ, fanya Zikr za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ.)

## Dhambi za miaka 80 zimesamehewa

Vile vile matumizi mengine ya ulimi ni kuendelea kutuma Swala na Salam kwa Mtume wetu kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم na kusamehewa dhambi, kama ilivyoelezwa katika *Durr-e-Mukhtar*: Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ atasamehe madhambi ya miaka 80 ya mtu anayetuma Sala kwa Mtume wetu Kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم mara moja na inakubaliwa.

*(Durr-e-Mukhtar, vol. 2, p. 284)*

## Hairuhusiwi kusema 'Bismillah ki-jiye'[1]

Baadhi ya watu wanasema '*Bismillah ki-jiye!*', '*Aao jee Bismillah*' au '*Mayn nay Bismillah ker daali*'.Kawaida wafanya biashara' mauzo ya kwanza ya siku yanaitwa kama 'Bauni' lakini watu wengine huita '*Bismillah*' vile vile.Kwa mfano, '*Mayri to aaj abhi tak Bismillah hi nahin huyi!*' Misemo hii yote si sahihi.Vivyo hivyo, mtu akifika wakati mtu anakula, mara nyingi mtu huyo husema, 'Njoo ule mlo pamoja nami.'Jibu linalopokelewa kwa kawaida ni, '*Bismillah*' or '*Bismillah ki-jiye!*'

Imeelezwa katika ukurasa wa 22, sehemu ya 16 ya Bahar-e-Shari'at, chapisho la Dawat-e-Islami, 'Ulama [Wanazuoni wa Kiislamu] wametangaza kwamba hairuhusiwi kabisa kusema 'بِسْمِ اللّٰه' kwa njia hii katika tukio kama hilo.' hata hivyo kauli hii inaweza kusemwa, 'soma 'بِسْمِ اللّٰه' na kula chakula.' Zaidi ya hayo, ni bora kufanya Du'a katika hafla kama hiyo.Kwa mfano, kusema, 'بَارَكَ اللّٰهُ لَنَا وَلَكُمْ', i.e.Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ akupe Baraka kwako na sisi, unaweza pia kusema kwa lugha ya mama yako (lugha yako ya asili): Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ akupe baraka.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب     صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

[1] Misemo kama hii hutumiwa kimakosa na watu wa bara katika nyakati tofauti.

## Wakati gani ni Kufr kusema 'بِسْمِ اللهِ'?

Kamwe, usisome بِسْمِ اللهِ' kabla ya kutenda Haramu na kitendo chochote kisichoruhusiwa. Ni Kufr kusoma بِسْمِ اللهِ' kabla ya kufanya kitendo chochote ambacho ni Haraam-e-Qat'ee [Haraam kabisa].Imeelezwa katika Fatawa 'Aalamgiri: Ni Kufr kusema 'بِسْمِ اللهِ' wakati wa kunywa mvinyo, kufanya zinaa au kucheza kamari. *(Fatawa 'Aalamgiri, vol. 2, p. 273)*

## Wakati gani ni dhambi kufanya Dhikrullah?

Kumbuka! Kufanya Zikr na kumswalia Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, ni matendo yenye malipo lakini katika baadhi ya hali yanakuwa haramu pia.Kwa mfano, katika ukurasa wa 533 wa juzuu ya 1 ya Bahar-e-Shari'at, chapisho la Maktaba-tul-Madinah, imeelezwa: Wakati wa kuonesha bidhaa kwa mteja, hairuhusiwi kwa mfanyabiashara kumswalia Mtume kipenzi na mwenye Baraka صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, au kusema 'سُبْحٰنَ اللهِ' kwa mteja kwa nia ya kuonyesha bidhaa kwa ubora wa juu.

Vile vile kwa kuona mtu yeyote wa kidini, hairuhusiwi kumswalia Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kwa nia ya kuwajulisha watu ujio wa mtu huyo ili watu wasimame wakimpa heshima na kuondoka katika nafasi zao. [kwa ajili yake]. *(Rad-dul-Muhtar, vol. 2, p. 281)*

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Nikizingatia hukumu hii, huwa nawaomba ndugu wa Kiislamu waepuke kusema 'Mwenyezi mungu' 'Mwenyezi mungu' kwa sauti kubwa nilipofika kwa

sababu inaonekana hii inalenga kukaribisha, sio kufanya Zikr za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ.

## Kuita Haleem [حَلِيْم] badala ya Khichra

Ndugu wapenzi wa kiislamu! Haleem [حَلِيْم] ni moja wapo ya majina hayo ya Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ ambayo inaelezea sifa zake.Kwa hivyo, ingawa inaruhusiwa kukiita chakula kama Haleem, mimi binafsi sikupenda.Chakula hiki pia huitwa Khichra kwa Kiurdu; kwa hiyo, ninatumia jina hili [i.e. Khichra] kwa muda mrefu iwezekanavyo.

Imetajwa katika *Tazkira-tul-Awliya*: Mara moja Sayyiduna Ba-Yazeed Bistami رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه alichukua tufaha jekundu mkononi mwake na kusema, 'Hili [tufaha] ni lateef sana [لَطِيْف].' Sauti ilisikika kutoka kwa Ghayb [i.e. Isiyoonekana], 'Je, hukuona haya kutumia Jina Letu kwa tufaha!' Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ aliondoa ukumbusho wake kutoka moyoni mwa Sayyiduna Ba-Yazeed Bistami رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه kwa siku arobaini.Sayyiduna Ba-Yazeed Bistami رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه pia aliapa kwamba hatakula matunda ya (mji wake) Bistaam. *(Tazkira-tul-Awliya, p. 134)*

Ulitambua! Maana moja halisi ya 'Lateef' ni 'bora' vile vile, lakini tangu 'لَطِيْف' ni jina la Mwewnyezi mungu عَزَّوَجَلَّ ambalo linaelezea moja ya sifa zake, Sayyiduna Ba-Yazeed Bistami رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه alionywa.

## Nyakati za malipo laki moja

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Kama tutatumia ulimi wetu kwa madhumuni sahihi, kwa hakika tunaweza kupata malipo zaidi na zaidi mara kwa mara.Imeelezwa katika Hadithi iliyobarikiwa: Kwa mtu anayefanya Zikr ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ sokoni, kutakuwa na Nuru [i.e. nuru] kwa kila unywele Siku ya Kiyama. *(Shu'ab-ul-Iman, vol. 1, p. 567)*

Kumbuka! Kusoma Quran Tukufu, Kusoma Hamdi na Kumsifu Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ, kufanya du'a na maombezi, kutuma salat na salam juu ya Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akisoma Na'at (Kasida) akitoa Mahubiri [i.e. Khutba za Kiislamu] na somo, kutoa Bayan yenye msukumo wa Sunnah, n.k. zote zimejumuishwa katika Dhikrullah.Kwa hiyo, kila ndugu wa Kiislamu anapaswa kuwasilisha somo za *Faizan-e-Sunnat* kwa angalau dakika 12 sokoni kila siku.Atapata malipo ya kufanya Zikrullah sokoni kwa muda wote anaotumia katika kutoa somo.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Ubora wa kutimiza hitaji na kuuliza juu ya afya ya mtu

سُبْحٰنَ اللّٰـه عَزَّوَجَلَّ! Wale ndugu wa Kiislamu na wadada wa Kiislamu wana bahati sana ambao wanazishika ndimi zao katika kuwalingania watu kwenye haki, kuwasilisha Bayan yenye msukumo wa Sunnah, kufanya Dhikr ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na kumswalia Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Ni kitendo cha

kupata malipo ya kutimiza haja ya Muislamu. Zaidi ya hayo, kumfariji mgonjwa au Muislamu mwenye matatizo pia ni matumizi makubwa [chanya] ya ulimi.

## Malipo makubwa ya kuuliza juu ya afya ya mtu

Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alisema: Mwenye kwenda kutimiza haja yoyote ya nduguye Muislamu, Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ humpa kivuli kupitia malaika 75,000. Malaika hao humfanyia Dua na anazama kwenye baraka mpaka amalize [kutimiza haja]. Akimaliza, Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ humuandikia malipo ya Hajj moja na 'Umra moja.Aliyeuliza baada ya mgonjwa, Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ atamwekea kivuli kupitia Malaika 75,000, angeliandikiwa jema moja kila anapoinua mguu wake mpaka atakapofika nyumbani, dhambi yake moja ingefutika kila anapoweka mguu wake na daraja moja ingenyanyuliwa. Atakapokaa na wagonjwa, baraka zitamfunika kabisa na baraka zitamfunika kabisa hadi atakaporudi nyumbani.

*(Al-Mu'jam-ul-Awsat, vol. 3, p. 222, Hadith 4396)*

Mtu hupata ujira mkubwa kwa kutumia ulimi wake kumfariji mtu ambaye mtoto wake anaumwa, asiye na kazi au mwenye deni, aliyepata ajali, ambaye mali yake huibiwa na mwizi, au dacoit (mshirika wa wizi wa kutumia silaha) ambaye anapata hasara katika biashara yake au yule anayekuwa na wasiwasi juu ya kupoteza kitu.Kwa ufupi, malipo makubwa hupatikana kwa kumfariji mtu anayepatwa na matatizo kutokana na sababu yoyote ile.

## Jozi ya mavazi ya Mbinguni

Imesimuliwa kutoka kwa Sayyiduna Jabir رَضِیَ اللهُ عَنْهُ kwamba Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alisema: Atakayetoa rambirambi zake kwa mtu mwenye huzuni, Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ atamfanya avae vazi la uchamungu na ataibariki nafsi yake miongoni mwa nafsi.Atakayetoa rambirambi zake kwa mtu mwenye matatizo, Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ atamfanya avae mavazi ya Mbinguni, mavazi mawili ambayo hata ulimwengu (mzima) hauwezi kuwa bei yao. *(Al-Mu'jam-ul-Awsat, vol. 6, p. 429, Hadith 9292)*

## Ulimi una faida na pia unadhuru

اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ! Kuna faida nyingi sana za kutumia ulimi ipasavyo.Hata hivyo, ulimi huu huu unakuwa sababu ya mateso makubwa ikiwa hautatumiwa kwa mujibu wa amri za Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ. Imesimuliwa kutoka kwa mtu mashuhuri Sahabi, Sayyiduna 'Abdullah Bin Mas'ood رَضِیَ اللهُ عَنْهُ kwamba Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alisema: Makosa mengi ya mtu yapo katika ulimi wake. *(Shu'ab-ul-Iman, vol. 4, p. 240, Hadith 4933)*

## Kila asubuhi sehemu za mwili huomba ulimi

Shaykh Sayyiduna Abu Sa'eed Khudri رَضِیَ اللهُ عَنْهُ amesimulia: Mtu anapoamka asubuhi, viungo vyake vyote vya mwili huuomba ulimi.Vinasema, 'Muogopeni Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ katika mambo yetu, kwa sababu tunahusishwa na wewe.Ukibaki sawa,

basi sisi nasi tutabaki sawa; lakini ukiwa mpotovu, basi sisi nasi tutakuwa wapotovu!' *(Sunan-e-Tirmizi, vol. 4, p. 183, Hadith 2415)*

Mfasiri mashuhuri, mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه amesema wakati akiifafanua Hadithi hii iliyobarikiwa: (Ewe ulimi!) Tumehusishwa na wewe katika manufaa na hasara, nafuu na faraja, na mateso na dhiki.Ikiwa utafanya vibaya, tutaingia kwenye shida.Ikiwa utatenda kwa haki, tutaheshimiwa.Kumbuka kwamba ulimi huakisi (hali ya) moyo.Wema na ubaya wake unaonyesha uzuri na ubaya wa moyo Ikiwa utafanya vibaya, tutaingia kwenye shida. *(Mirat, vol. 6, p. 465)*

## Matatizo yanayosababishwa na matumizi mabaya ya ulimi

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Nyakati fulani, kutumia ulimi bila uangalifu husababisha matatizo makubwa.Ikiwa mwanamume atatamka Talaka, Talaka, Talaka, kwa ulimi huu kwa mkewe ambaye ameingia naye, Talaaq-e-Mughallazah itatokea.Wakati fulani, hupelekea hata kuua ikiwa ulimi huu unatumiwa kumtukana mtu jambo ambalo huchochea hasira yake.Iwapo mtu atatumia ulimi huu kumkemea Muislamu bila ya sababu yoyote ya kisheria na ikamdhuru hisia zake, basi hakika ni dhambi na inaongoza kuelekea Motoni.

Imesimuliwa katika kitabu '*Tabarani*' kwamba Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alisema, 'Yule ambaye amemuudhi Muislamu

(bila ya sababu yoyote ya kisheria) ameniudhi mimi, na aliyeniudhi, amemkasirisha Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ.'

*(Al-Mu'jam-ul-Awsat, vol. 2, p. 386, Hadith 3607)*

## Furaha ya milele na karaha

Sayyiduna Bilal Bin Haaris رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہُ amesimulia kwamba Mtume mtukufu صَلَّی اللّٰہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema: Mtu anazungumza jambo jema bila ya kujua mipaka yake, basi ataandikiwa radhi za Mwenyezi Mungu mpaka siku atakayokutana naye.Na mtu mmoja anazungumza ubaya bila ya kujua mipaka yake, basi Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ huandika adhabu yake mpaka siku atakapokutana naye. *(Mishkat-ul-Masabih, vol. 2, p. 193, Hadith 4833; Sunan-ut-Tirmizi, vol. 4, p. 143, Hadith 2326)*

Mfasiri mashuhuri, mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan رَحۡمَۃُ اللّٰہِ عَلَیۡہ amesema wakati akifafanua Hadithi hii iliyobarikiwa: (Wakati fulani, mtu) husema jambo baya ambalo Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ atamkasirikia milele. Kwa hiyo, mtu anapaswa kuzungumza baada ya kuzingatia kwa makini. Sayyiduna 'Alqamah رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ walikua wakisema kwamba [zilizotajwa hapo juu] hadithi za Bilal Ibn Haaris رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ hunizuia [kusema] mambo mengi, i.e.natamani kuzungumza kitu lakini [kisha] naikumbuka Hadithi hii na kukaa kimya. *(Mirat, vol. 6, p. 462)*

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Kuzungumza bila kufikiri kunaweza kuwa na madhara makubwa sana na kunaweza kumchukiza Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ milele. . Hakika amani na

usalama upo katika kuweka Qufl-e-Madinah (i.e. walinzi wa Madani) kwenye ulimi. Ni jambo la manufaa sana kuwa na mazungumzo kwa njia ya maandishi au lugha ya ishara kwa ajili ya kuwa na mazoea ya kukaa kimya kwa sababu mtu, ambaye anazungumza zaidi, kwa kawaida hufanya makosa zaidi na hata kufichua siri. Pia ni vigumu sana kwa mtu kama huyo kujiepusha na madhambi kama kusengenya, tale-telling na kutafuta makosa (ya watu). مَعَاذَ اللّٰه Wakati mwingine mtu muongeaji hata hutamka Kufr.

## Matokeo ya ugumu wa moyo

Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ atuhurumie na atujaalie tuudhibiti ulimi wetu kwani ulimi unasababisha ugumu wa mioyo pia, kwa kuzungumza bila ya lazima na kughafilika katika kufanya Dhikrullah. Mtume mtukufu صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: Kutumia lugha chafu kunatokana na ugumu wa moyo na ugumu wa moyo uko kwenye moto. *(Sunan-ut-Tirmizi, vol. 3, p. 406, Hadith 2016)*

Mtu mashuhuri mtoa maoni, mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema wakati akifafanua Hadithi hii iliyobarikiwa: Ina maana kwamba kama mtu atatumia ulimi wake bila woga na kusema kila jambo jema au baya bila kufikiri, basi hii inaashiria kuwa yeye ni mgumu wa moyo na hana adabu.Ugumu ni ule mti ambao mzizi wake upo ndani ya moyo wa mtu na tawi lake (lipo) Motoni.

Mtu huyo asiye na woga huishia kuwa Kafir [i.e. asiyekuwa Muislamu] kwa kukosa heshima hata katika mahakama ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na kipenzi chake Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم.

*(Mirat-ul-Manajih, p. 641, vol. 6)*

## Kusagwa ulimi!

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Hakika ni hatari sana kuzungumza kupita kiasi, kama wakati mwingine مَعَاذَ اللّٰه; kuzungumza bila ya lazima kunaweza kumfanya mtu afanye kufr [i.e. kutoamini].Laiti watu wangefanya mazoea ya kutafakari maneno kabla ya kuyasema kwamba maneno haya yataleta manufaa gani katika maisha yetu ya baadaye.Ikiwa hakuna manufaa yoyote [ya Akhera], basi badala ya kuongea, mswalie Mtume Kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kwa muda huo makhsusi kwani itakunufaisha sana huko Akhera!

Imeelezea katika *Asraar-ul-Awliya*: Mara moja Sayyiduna Haatim Asam رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه Alisema jambo lisilo la lazima kwa ulimi wake alioupenda. Alijuta رَحْمَةُ الله عَلَيْه na kuuweka ulimi wake katikati ya meno kwa nguvu kiasi cha kuanza kuvuja damu! Zaidi ya hayo, hakuzungumza na yeyote (isiyo lazima) hadi miaka ishirini kama kafara ya [kusema] kauli hii moja isiyo ya lazima! *(Asraar-ul-Awliya, p. 33)*

Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ amhurumie na atusamehe kwa ajili yake!

اٰمِيْن بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

## Mtu anapaswa kufanya nini juu ya kusema kitu bila ya lazima?

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Je, ulitambua! Sayyiduna Haatim Asam رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه alijuta sana kusema kauli isiyo ya lazima na kuuponda ulimi wake! Kumbuka hukumu hii ya Kiislamu kwamba Sheria hairuhusu kujiumiza nafsi yako katika hali ya fahamu.Kwa hiyo, katika mifano kama hii, tutafsiri kwamba watakatifu waliobarikiwa wamejiumiza katika hali ya kukosa fahamu, kama '*Hosh mayn jo na ho woh kya na karay*' i.e. 'mtu ambaye hana fahamu anaweza kufanya lolote bila kujua.'

Hata hivyo, ilikuwa sifa ya pekee ya watakatifu hao waliobarikiwa Ikiwa tu watu angalau wangesema 'Mwenyezi mungu, 'Mwenyezi mungu' mara 12 au kumswalia Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, mara moja kama kafara ya kutamka chochote bila ya lazima. Kwa njia hii, pengine Shetani hatatuhimiza tuzungumze bila ya lazima, akiogopa kwamba tunaweza kumsumbua kwa kufanya Zikr na kumswalia Mtume kipenzi na Mwenye baraka صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم!



www.dawateislami.net

Imepokewa katika **Minhaj-ul-'Aabideen**: Zikrullah ni chungu kwa Shetani kama mateso anayoyapata mtu kwa ajili ya [maradhi ya] Aakilah. *(Minhaj-ul-'Aabideen, p. 46)*

Aakilah ni ugonjwa unaoathiri nyama ya binadamu kwa namna ambayo huanza kujitenga na mwili pekeake.

## Mifano 14 ya sentensi zisizo za lazima

Kwa kusikitisha, kampuni ya watu wema ni adimu kupatikana siku hizi. Kwa bahati mbaya, watu wengi wanaoonekana kuwa wazuri inaonekana wanazingatiwa wakizungumza bila lazima, badala ya kuzungumza kitu kizuri.Kama tu watu wangekutana na watu wenye lengo pekee la kumridhisha Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ. Kama tu watu wangezungumza tu kwa lazima wanapokutana na watu.

Kumbuka! Sio Haraam [i.e. marufuku] au dhambi ya kuzungumza isivyohitajika au kuongeza maneno zaidi kwenye mazungumzo ya lazima. Hata hivyo, ni bora kuepuka. *(Ihya-ul-'Uloom, vol. 3, p. 143)*

Wakati akizungumza pasipo ulazima, kuna uwezekano mkubwa kwamba mtu akajiingiza katika mazungumzo ya 'dhambi'. Kwa hiyo, amani na usalama hutegemea kukaa kimya. Katika jamii zetu, siku hizi maswali kama hayo mara nyingi yanaulizwa bila ya lazima jambo ambalo humfanya mtu mwingine aone aibu na anaweza hata kufanya dhambi ya kusema uwongo ikiwa atayajibu bila tahadhari. Maswali haya wakati mwingine huulizwa kwa

makusudi. Katika hali kama hizi, maswali haya hayawezi kuchukuliwa kuwa "yasiyo ya lazima". Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya sentensi kama hizo. Hakuna ubaya ikiwa maswali haya yanaulizwa kwa sababu. Hata hivyo, walinde Waislamu kutokana na kufedheheka au kutenda dhambi kwa kuepuka maswali hayo kadiri inavyowezekana. Kwa mfano:

1. Nini kinatokea!
2. Usifanye dua [kwa ajili yangu] siku hizi!
3. Ewe ndugu! umechukizwa [na mimi]?
4. Nadhani hujafurahia!
5. Gari hili lilikugharimu kiasi gani?
6. Ni mfano gani wa gari lako?
7. Gharama ya nyumba katika eneo lako ni kiasi gani?
8. Mfumuko wa bei uko juu kweli!
9. Hali ya hewa ikoje uko?
10. Oh, hali ya hewa ni ya joto sana!
11. Kuna baridi sana sikuhizi.
12. Je, itaacha kunyesha!
13. Usambazaji wa umeme ulikatishwa mara tu mvua ilipoanza kunyesha!
14. Je, kulikua na usambazaji wa umeme nyumbani kwako au la?

Sentensi hizi na zingine nyingi kama hizi husemwa bila lazima. Hata hivyo, mtazamo hasipaswi kuundwa kwa mtu anayezizungumza sentensi kama hizo. Badala yake, dhana nzuri inapaswa kufanywa kwani mtu anayesema sentensi kama hiyo ambayo inaonekana kuwa sio lazima, anaweza kuwa na sababu nzuri ya kuifanya ambayo haujaelewa. Zaidi ya hayo, mtu kama huyo si mtenda dhambi hata kama swali au sentensi si ya lazima.

## Mifano 13 ya maswali yasiyo ya lazima yaliyoulizwa kutoka kwa Hujjaj[1]

Ndugu na marafiki kwa kawaida huuliza maswali mbalimbali yasiyo ya lazima hata kutoka kwa Hujjaj wanaorejea kutoka Madina. Ifuatayo ni mifano yao 13:

1. Je ulikumbana na ugumu wowote wakati wa safari?
2. Ingekua hivyo kungekua na watu wengi sana!
3. Kulikua na mfumuko wa bei?
4. Ulipata malazi mazuri au la?
5. Je!makazi yako yalikua karibu na haramu au mbali nayo?
6. Hali ya hewa ilikuaje huko?
7. Je, hali ya hewa ilikua ya joto sana huko?
8. Ulifanya Tawaf mara ngapi kila siku?
9. Je, umefanya Umrah mara ngapi?

[1] Wingi wa Hija - Mtu ambaye amehiji.

10. Je, umenifanyia dua kwa wingi uko Makkah au la?
11. Je, hema lako lilikua karibu na Jamrat huko Mina au mbali?
12. Ulikaa Madinah kwa siku ngapi?
13. Je, ulisema salamu yangu uko Madinah, haswa kwa kutaja jina langu?

Ingawa mifano iliyotajwa hapo juu ya maswali hairuhusiwi, tafakari kuhusu madhumuni yao kabla ya kuuliza. Usiulize [maswali kama hayo] ikiwa hakuna haja yoyote kwa sababu baadhi ya haya yanaweza kumfanya Haji ahisi aibu, mengine yanaweza kumfanya awe na wasiwasi na mengine yanaweza kumfanya atende dhambi ya kusema uwongo ikiwa atayajibu bila tahadhari. Kwa hiyo, 'Kimya ni dhahabu'.

## Mifano 4 ya sentensi mbaya au za dhambi

Baadhi ya watu wazungumzaji hawaepuki kusema hata sentensi za dhambi na zile sentensi ambazo wanatoa tuhuma za uwongo dhidi ya wengine bila uthibitisho wowote. Ifuatayo ni mifano yao 4:

1. Jumuiya yetu (au kijiji kizima) kimekua cha wazushi. Ni mimi pekee niliyebaki salama kutokana na uzushi (lakini si kweli kwa ujumla kwani wazee, wanawake na watoto Zaidi hubaki salama kutoka humo).
2. Watumishi wetu wote wa serikali wanapokea rushwa.

3. Wafanyakazi wote wa kampuni ya usambazaji wa umeme ni watu waovu, مَعَاذَاللّٰہعَزَّوَجَلَّ.
4. Kila mtu serikalini ni mwizi.

## Mifano 19 ya maswali yasiyo ya lazima yaliyoulizwa siku ya Eid-ul-Adha

Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya maswali yasiyo ya lazima yaliyoulizwa siku ya Eid-ul-Adha bila madhumuni yoyote:

1. Utanunua ng'ombe lini?
2. Gharama ya wanyama ingekua juu siku hizi!
3. Ulinunua ng'ombe kwa kiasi gani?
4. Ng'ombe wako ana afya nzuri sana!
5. Ng'ombe wako ana umri gani?
6. Ng'ombe wako ni mkali?
7. Je, ng'ombe wako ulimtembeza nyumbani au ulimsafirisha?
8. Ulitumia kiasi gani kumsafirisha ng'ombe wako?
9. Utamchinja lini?
10. Je, mchinjaji alikuja kwa wakati au la?
11. Mchinjaji aliondoka baada ya kuchinja na kurudi akiwa amechelewa sana.

12. Uko sahihi! Wachinjaji walitupotezea muda kwa kuchelewa kufika.
13. Nilifurahia sana kuona ng'ombe akikimbia udhibiti wa mchinjaji!
14. Uko sahihi! Mchinjaji hakuwa mtaalamu! (Inaweza kuwa kusengenya, shutuma za uwongo, dhana mbaya au inaweza kuumiza hisia za mtu huyo na dhambi zingine kama hizo zinaweza kutendwa. Hata hivyo, hakuna ubaya katika sentensi hii ikiwa mchinjaji huyo kweli si mtaalamu na kwa kumfahamisha mtu. mtu anakusudia kumwokoa kutoka kwa mchinjaji huyo.)
15. Mbuzi wako ana umri gani?
16. Ulinunua mbuzi kwa kiasi gani?
17. Oh, umenunua ghali sana.
18. Je, hata kutembea au la?
19. Mchinjaji alitoza kiasi gani kuchinja? nk., nk.

## Mifano 5 ya mazungumzo yasiyo ya lazima yaliyofanywa wakati wa kuzungumza kwenye simu

Maswali yasiyo ya lazima mara nyingi huulizwa wakati wa kuzungumza kwenye simu pia. Ifuatayo ni mifano yao 5:

1. Unafanya nini?

2. Uko wapi?
3. Mtu akimwita mtu akiwa ndani ya gari, mara nyingi swali lifuatalo huulizwa, 'Ni nani mwingine anafuatana nawe?'
4. Unapita wapi?
5. Umefikia wapi?

Hata hivyo, swali lililoulizwa kimakusudi halitachukuliwa kuwa swali lisilo la lazima lakini baadhi ya maswali yanaweza kumfanya mtu aone haya na kusema uwongo. Kwa mfano, mtu anaweza asiweze kutoa majibu sahihi ya maswali 1-2-3 yaliyotajwa hapo juu kwani anaweza kutaka kuficha kwamba anafanya nini, yuko wapi au ni nani mwingine yuko naye. Amani na usalama katika maneno yote mawili upo katika kuzungumza kwa makusudi tu na si Zaidi ya lazima.

## Mifano14 ya maswali yanayomlazimisha mtu kusema uwongo

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Nyakati nyingine watu huuliza maswali ambayo yanaweza kumfanya mtu aseme uwongo ikiwa anajibu bila tahadhari au ikiwa kusema ukweli kunaweza kumuaibisha muulizaji. Ijapokuwa mtu anayeuliza maswali hayo si dhambi lakini ni bora kujiepusha na maswali haya bila ya lazima ili kuwaokoa Waislamu kutenda madhambi. Ifuatayo ni mifano 14 ya maswali kama hayo:

1. Je, ulikuwa na tatizo lolote katika kutafuta nyumba yetu?
2. Je, ulipenda chakula tulichohudumia?
3. Chai niliyotengeneza ilikuwaje?
4. Je, uliipenda nyumba yetu?
5. Je, unanifanyia Du'a au la?
6. Bayan ilikuwaje [i.e. hotuba] niliyotoa hivi punde?
7. Sauti yangu ilikuwaje nilipokuwa nikisoma Na'at?
8. Je, nilichosema kilikuumiza?
9. Je, umesumbuliwa kwa ziara yangu?
10. Ninakuchosha?
11. Je, nilikatiza mazungumzo yako?
12. Je, umechukizwa na mimi?
13. Nimekufurahisha?
14. Je, nimewahi kuumiza hisia zako?

## Maneno hatari zaidi yasiyo ya lazima

Watu wengine ni wa ajabu sana. Wanatamani kutiwa moyo bila sababu yoyote katika chochote wanachosema. Kwa mfano:

1. Kwa hiyo umeelewa nini?
2. Je, umeelewa nilichosema? (Hata hivyo, wakati mwingine swali hili ni la manufaa pia ikiwa walimu wa kidini au watu

wa kidini, nk. iulize kwa makusudi kutoka kwa wanafunzi au wasaidizi wao ili waweze kuieleza [tena] kwa wale ambao bado hawajaelewa. Katika hali hii, watu hawapaswi kujibu kwa njia ya kupotosha katika uthibitisho, ikiwa kwa kweli hawajaelewa jambo hilo.)

3. Hivyo ni sawa?
4. Je, nina makosa?
5. 'Nini maoni yako?' Mtu huyo hana chaguo ila kujibu kwa uthibitisho hata kama hakubaliani na kauli ya muulizaji. Kwa njia hii, dhambi ya kusema uwongo hufanywa mara nyingi.

Ikiwa huna ujasiri wa kuwarekebisha watu hao wazungumzao, basi amani na usalama unatokana na kukaa mbali nao kwani kujibu kwa uthabiti mazungumzo yao ya dhambi kunaweza kusababisha kuelekea Motoni! Pia inazingatiwa kuwa watu waongeaji hivyo wakati mwingine hutoa kauli za kupotosha, مَعَاذَ اللّٰه عَزَّوَجَلَّ hata Kufr na kutaka kutiwa moyo, kuwauliza wengine, 'Kwa hiyo, niko sawa?' Kupata jibu la uthibitisho kwa njia hii, wakati mwingine hata huwafanya wengine kufanya ukafiri [i.e. kutoamini] kwa sababu pia ni Kufr kuidhinisha Kufr katika fahamu. اَلْعِيَاذُ بِاللّٰه عَزَّوَجَلَّ

*Ay kash! Zarurat kay siwa kuch bhi na boloon*
*Allah zaban ka ho 'ata Qufl-e-Madinah*

## Ufafanuzi wa "taarifa isiyo ya lazima"

Ikiwa neno moja linatosha kuwasilisha maana wakati wa mazungumzo, basi kutumia neno la pili la nyongeza 'si lazima'.

Hujjat-ul-Islam, Sayyiduna Imam Muhammad Bin Muhammad Ghazali رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه amesema katika *Ihya-ul-'Uloom*: Kama neno moja linatosha kufikia lengo (la mzungumzaji) na akatumia maneno mawili, basi neno hili la pili litazingatiwa kuwa si la lazima. Ina maana kwamba itakuwa zaidi ya inavyotakiwa [kufikia lengo] na neno lolote ambalo ni zaidi ya mahitaji, ni la kulaumiwa. *(Ihya-ul-'Uloom, vol. 3, p. 141)*

Kama lengo halitimizwi kwa neno moja, basi maneno mawili au zaidi yanayosemwa kulingana na mahitaji sio lazima. Hata hivyo, kauli hiyo ingezingatiwa kuwa sio lazima ambayo haina maana. Neno au kauli si lazima ikiwa inasemwa kimakusudi wakati ulazima au hitaji linapotokea au kupata manufaa yoyote. Wakati mwingine, maneno yaliyoongezwa ili kufanya hotuba isikike vizuri pia sio lazima. Kwa mfano, vina na mashairi hayo si ya lazima ambayo yanatumiwa kimakusudi kuipamba Bayan, uandishi au ushairi. Maneno hayo pia si ya lazima ambayo wakati mwingine yanapaswa kuongezwa au kuondolewa kulingana na akili ya msikilizaji.

Watu wanaweza kugawanywa katika makundi matatu kulingana na akili zao:

1. Mwenye akili sana.
2. Mwenye akili kiasi.



www.dawateislami.net

3. Mwenye akili dhaifu.

Kwa mtu mwenye akili nyingi, neno moja wakati fulani linatosha kuelewa kikamilifu kile kinachosemwa ambapo ni vigumu kwa mtu mwenye akili nyingi kuelewa [jambo] bila maelezo yake. Mwenye akili dhaifu wakati mwingine hawezi kuelewa chochote hata akielezwa mara kumi. Kwa mujibu wa uainishaji huu, kumbuka kwamba neno la pili litachukuliwa kuwa si la lazima ikiwa linatumiwa kuelezea jambo lile lile kwa mtu ambaye tayari amelielewa kwa neno moja. Vivyo hivyo, ikiwa mtu mwenye akili nyingi anaelewa [jambo] katika maneno 12, basi neno lolote la ziada linalotumiwa bila kusudi kuelezea jambo lile lile litaonekana kuwa si la lazima.

Zaidi ya hayo, ikiwa mtu mwenye akili dhaifu haelewi kitu isipokuwa maneno 100 yametumika, basi hata maneno haya mia hayatachukuliwa kuwa hayana ulazima kwa vile yametumika kwasababu. Kwa kujumlisha, neno moja lililotamkwa zaidi ya maneno ya kutosha kufikia lengo, sio lazima. Pia itazingatiwa kuwa si lazima kutamka 'neno moja' la kauli ambayo inaruhusiwa lakini haina maana. Ikiwa kauli hiyo haijuzu, kutamka hata 'neno lake moja' kutazingatiwa kuwa ni jambo lisiloruhusiwa na ni dhambi.

## Yule ambaye anamwamini Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ na maisha ya baadae

Baada ya kupitia maelezo yaliyotajwa hapo juu, inaweza kutokea kwako kwamba ni vigumu sana kujiepusha na kuongea bila

sababu.Usipoteze tumaini na endelea kujaribu. Kuwa na mazoea ya kuweka Qufl-e-Madinah kwenye ulimi (yaani kukaa kimya), jaribu kuwa na mazungumzo kwa njia ya maandishi au lugha ya ishara ikiwezekana, kwani juhudi za dhati zitakuongoza kuelekea kule unakoenda. Inasemekana kwamba, 'اَلسَّعْيُ مِنِّيْ وَالْاِتْمَامُ مِنَ اللّٰہ' i.e. kazi yangu ni kufanya juhudi; mafanikio yanatolewa na Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ. Kukariri hadithi zifuatazo *Sahih Bukhari* itakuwa na manufaa makubwa kwa kuwa na mazoea ya kukaa kimya, اِنْ شَآءَاللّٰہ. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alisema, 'mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na maisha ya baadae; aseme [jambo] jema au anyamaze.' *(Sahih Bukhari, vol. 4, pp. 105, Hadith 6018)*

## Watu wa ajabu wa kuongea

Kujiingiza katika tabia hiyo ya mazungumzo yasiyo ya lazima, watu wengine pia huwafanya warudie kile wanachosema wengine! Labda pia umefanya kosa lile lile bila kukusudia, kwa hivyo litafakari! Ufuatao ni mfano wa kumfanya mtu arudie alichosema: Zayd anasema kitu kwa Bakr. Ingawa Bakr ameielewa, anajifanya kwamba hajaielewa. Anainua kichwa chake kwa kuuliza na mara nyingi maneno haya hutamkwa kwa kuhoji: 'ahaa?' 'ndio?' 'nini'? Kwa njia hii, Zayd anafanywa kurudia bila sababu yoyote aliyoyasema hivi punde.

Tangu Ameer-e-Ahl-e-Sunnat دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَه ana uzoefu na tabia hii ya baadhi ya watu, huwa anakaa kimya badala ya kurudia alichosema, kujibu ishara hizo za kuhoji.Matokeo yake, inaonekana kwamba msikilizaji alikuwa tayari ameelewa mara



www.dawateislami.net

moja! Juhudi kubwa zinahitajika ili kuondokana na tabia zisizo za lazima. karibu haiwezekani kuondokana na tabia kama hiyo mara moja baada ya kusikiliza hotuba moja (au kusoma baadhi ya maudhui muhimu). Tafakari kwa kina na ujiandae kiakili kwamba hutatamka maneno kama 'huh', 'nini', n.k mara tu baada ya kusikiliza mtu fulani amesema. Hata hivyo ukisahau [na kutamka maneno kama hayo], tekeleza uwajibikaji wako.

## Kuchambua mazungumzo

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Ifuatayo ni simulizi inayoelezea uangalifu uliozingatiwa na watakatifu waliobarikiwa رَحِمَهُمُ اللّٰهُ wakati wa mazungumzo.

Imeelezwa katika '***Minhaj-ul-'Aabideen***': Mara moja Sayyiduna Fudayl Bin 'Iyaad رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه alikutana na Sayyiduna Sufyan Sawri رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه. Wote wawili walilia baada ya mazungumzo.Basi Sayyiduna Sufyan Sawri رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه alisema, 'Ewe Abu 'Ali (hii ni Kunyah ya Sayyiduna Fudayl)! Natarajia zawadi kubwa kwa mkutano huu wa leo.' Sayyiduna Fudayl Bin 'Iyaad رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه akasema, 'Ninaogopa sana mkutano huu wa leo.' Sayyiduna Sufyan Sawri رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه akauliza, 'kwa nini?' Sayyiduna Fudayl رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه akajibu, 'Si sote wawili hatukurembesha mazungumzo yetu? Je! hatukujaribu kufanya mazungumzo yetu yasikike vizuri zaidi?' Kuisikiliza, Sayyiduna Sufyan Sawri رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه akaanza kulia. *(Minhaj-ul-'Aabideen, p. 44)*

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Tunapaswa kutafakari juu yake. Hawa watu wema walikuwa wakikutana [wao kwa wao] kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ. Mazungumzo yao yalikuwa ni kwa mujibu kamili wa mafundisho ya Kiislamu. Hata hivyo walimcha Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ sana! Watakatifu wote wawili waliobarikiwa walikuwa wakilia kwa hofu kwamba wanaweza kuwa wamemuasi Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ wakati wa kuzungumza au wangeweza kusema sentensi nzuri bila lazima! Watu hao wanapaswa kujifunza kutokana nayo, ambao wanajidai; mara nyingi hutumia maneno magumu, nahau na mashairi ya lugha za Kiarabu, Kiajemi na Kiingereza wanapozungumza kwa Kiurdu, ili kuwavutia watu na ujuzi wao.

Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, ‘siku ya hukumu, Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ hatakubali Fard wala Nafl ya mtu anayejifunza kuzungumza kwa hila kwa nia ya kuziteka nyoyo za wanaume au za watu kwa njia hiyo.’

*(Sunan Abi Dawood, vol. 4, p. 391, Hadith 5006)*

Huku akielezea hii hadithi, Muhaddis mkuu, ‘Allamah Shaykh ‘Abdul Haq Muhaddis Dihlvi رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه amesema: ‘صَرْفُ الْكَلَامِ’ (i.e. kuzungumza kwa hila) [hapa] ina maana ya kusema uwongo kwa kujifanya ili kufanya mazungumzo yavutie, na kuyabadilisha kwa ajili ya kuleta mashaka na utata.

*(Ashi’a-tul-Lam’aat, vol. 4, p. 66)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Niruhusu nipate fursa ya kutaja ubora wa Sunnah kwa baadhi ya Sunna na adabu, kuhitimisha hotuba. Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mwenye kupenda Sunnah yangu ananipenda mimi na anayenipenda, atakuwa pamoja nami katika Jannah.'

*(Mishkat-ul-Masabih, vol. 1, p. 55, Hadith 175)*

*Seenah tayri Sunnat ka Madinah banay Aqa*
*Jannat may parausi mujhay tum apna banana*

*Moyo wangu uwe Madinah ya Sunnah yako, Ewe mpendwa*
*peponi, nipe nafasi katika ujirani wako*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Lulu za Madani 12 kuhusu kuingia na kutoka nyumbani

1. Unapotoka nyumbani soma Dua hii:

بِسْمِ اللّٰهِ تَوَكَّلْتُ عَلَى اللّٰهِ وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ اِلَّا بِاللّٰهِ

**Kwa jina la Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ, nimeweka Imani yangu ndani ya Mwenyezi mungu, hakuna hila wala haluna nguvu au uwezo isipokuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ.**

*(Sunan Abi Dawood, vol. 4, p. 420, Hadith 5095)*

اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ, kwa fadhila za kusoma Du'a hii, utakaa kwenye njia iliyonyooka, utalindwa na majanga, na utapata nusura ya Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ.

2. Dua ya kuingia nyumbani ni:

اَللّٰهُمَّ اِنِّیْۤ اَسْاَلُكَ خَيْرَ الْمَوْلَجِ وَ خَيْرَ الْمَخْرَجِ

بِسْمِ اللّٰهِ وَلَجْنَا وَ بِسْمِ اللّٰهِ خَرَجْنَا وَ عَلَى اللّٰهِ رَبِّنَا تَوَكَّلْنَا

**Ewe Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ! Ninakuomba, kwa wema wa kuingia na kutoka, tunaingia (nyumbani) tukianza na jina la Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ na toka (nyumbani) ukianza na jina la Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na tunaweka imani yetu kwa mola wetu, Mwenyezi mungu عَزَّوَجَلَّ.**

*(Sunan Abi Dawood, p. 420, vol. 4, Hadith 5096)*

Baada ya kusoma Du'a hii, wasalimie watu wa nyumbani kwako, kisha wasilisha Salam yako kwa Mtume Kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, kisha usome Sura Al-Ikhlas. Kutakuwa na baraka katika riziki yako na utabaki salama kutokana na migogoro ya nyumbani, اِنْ شَآءَاللّٰه.

3. Sema Salam kwa Maharim na Mahrimaat (k.m. mama yako, baba yako, kaka zako, dada zako n.k.) unapoingia na kutoka nyumbani.

4. Mtu anapoingia nyumbani bila kulisoma jina la Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ, kwa mfano, bila ya kusoma 'بِسۡمِ اللّٰه' shetani nae huingia pamoja nae.

5. Ukiingia katika nyumba iliyo wazi (hata ikiwa ni nyumba yako mwenyewe), basi sema:

اَلسَّلَامُ عَلَيۡنَا وَعَلٰى عِبَادِ اللّٰهِ الصّٰلِحِيۡنَ

**Salamu ziwe juu yetu na juu ya waja wema wa Mwenyezi Mungu.**

*Malaika wataijibu Salam hii.*

*(Rad-dul-Muhtar, vol. 9, p. 682)*

Kwa vile roho tukufu na yenye baraka za Mtume صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم rehema na amani ziwe juu yake, ipo kwenye nyumba za Waislamu, unaweza pia kusema yafuatayo:

اَلسَّلَامُ عَلَيۡكَ اَيُّهَا النَّبِيُّ

**Ewe mtume صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم! Salamu iwe juu yako.**

*(Bahar-e-Shari'at, part. 16, p. 96; Sharh-ush-Shifa, vol. 2, pp. 118)*

6. Unapotaka kuingia nyumbani kwa mtu, sema, 'Amani iwe juu yako', 'اَلسَّلَامُ عَلَيۡكُمۡ', naweza kuingia?

7. Ikiwa ruhusa haijatolewa ya kuingia nyumbani, rudi kwa furaha. Labda mkazi wa nyumbani anaweza kukataa kwa sababu ya hali fulani isiyoweza kuepukika.

8. mtu anapobisha mlangoni kwako, ni Sunnah kuuliza: Ni nani huyo? Mtu aliye nje anapaswa kusema jina lake. Kwa mfano, 'Muhammad Ilyas'. Si Sunnah kusema: 'Madinah!' 'Ni mimi!' 'Fungua mlango,' na sentensi nyingine zinazofanana na hizo kwenye tukio kama hilo badala ya kusema jina.

9. Simama mbali na mlango hadi upande mmoja baada ya kuwaambia jina lako. Hii itakuzuia kutazama ndani mara moja mlango unapofunguliwa.

10. Hairuhusiwi kuchungulia ndani ya nyumba ya mtu. Mbele ya nyumba za watu wengine, kuna nyumba za watu wengine katika ngazi ya chini.Kwa hivyo, ni lazima mtu awe mwangalifu anapotazama nje kutoka kwenye balcony [au dirisha] ili kuhakikisha kwamba haangalii ndani ya nyumba zao.

11. Unapotembelea nyumba ya mtu, usikosoe isivyo lazima mipango aliyoifanya kwani hii inaweza kuumiza hisia zake.

12. Baada ya kuondoka, fanya Du'a kwa ajili ya watu wa nyumbani, washukuru, wasalimie na wape zawadi ya



www.dawateislami.net

msukumo wa Sunnah wa kijitabu, kitabu, DVD, nk.kama inawezekana.

Kujifunza maelfu ya Sunah juu ya mada mbalimbali, nunua na usome vitabu viwili vilivyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah:

1. Kurasa ya 312-kitabu cha *Bahar-e-Shari'at*, sehemu ya 16.

2. Kurasa ya 120-kitabu cha *Sunnatayn aur Adaab*.

Mojawapo ya njia bora za kujifunza Sunan ni kusafiri na Madani Qafilahs ya Dawat-e-Islami pamoja na waja wa Mtume kipenzi.

*Seekhnay Sunnatayn Qafilay mayn chalo*
*Lootnay rahmatayn Qafilay mayn chalo*

*Haun gi hal mushkilayn Qafilay mayn chalo*
*Pao gey barakatayn Qafilay mayn chalo*

*Kujifunza Sunan, safiri na Madani Qafilah*
*Kupata rehma safiri na Madani Qafilah*

*Kutatua shida zako safiri na Madani Qafilah*
*Kupata Baraka safari na Madani Qafilah*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب     صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

## Kwa ajili ya kuwa muislamu mcha mungu na mwenye kusimamisha sala

Pitisha usiku wako kwenye jitimai ya kuhuisha Sunna ya Dawat-e-islami inayofanyika kila siku ya Alkhamis Kuamkia ijumaa ndani ya mji wako kwa nia ya kutaka radhi za Allah عَزَّوَجَلَّ pamoja na nia zingine nzuri. Ili upate kujifunza sunna kuwa na kawaida ya kusafiri siku 3 katika Madani Qafilah pamoja na Wapenzi wa Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم.

Fanya Fikr-e-Madina kwa kujaza kitabu cha Madani In'amat na ukipeleke kwa Zimmedar (msimamizi) wa eneo lako tarehe mosi ya kila mwezi wa Madani.

**Lengo langu la Madani:** 'Nitajitahidi kujirekebisha mwenyewe na watu wa ulimwengu mzima اِنْ شَآءَ اللّٰه عَزَّوَجَلَّ.

Kwa ajili ya kujirekebisha wenyewe tunatakiwa tuzifanyie kazi Madani In'amat na kwa ajili ya kuwarekebisha watu wa ulimwengu mzima tunatakiwa tusafiri katika Madani Qafilah.



Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan
UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 7213
Web: www.maktabatulmadinah.com | E-mail: feedback@maktabatulmadinah.com